

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA NNE

22 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA NNE – TAREHE 22 APRILI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA NISHATI NA MADINI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

159. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza Miradi ya TACTIC iliyopangwa kutekelezwa katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara.

160. MHESHIMIWA CHRISTINA SOLOMON MNDEME (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inawafikia Wanawake wote wenye uhitaji wa Mikopo katika Mkoa wa Tabora.

161. MHESHIMIWA CLAYTON REVOCATUS CHIPANDO (KIGOMA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza mtandao wa Barabara za lami Kigoma Mjini kwa kuongeza bajeti.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

162. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali haioni haja ya kufanya ZEMA kuwa Wakala wa NEMC ili kuratibu na kusimamia kwa ufanisi Miradi inayotekelezwa upande wa Zanzibar.

WIZARA YA ELIMU, SANYANSI NA TEKNOLOJIA:

163. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (MISSENYI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini ujenzi wa Chuo cha VETA Wilaya ya Missenyi utakamilika ikizingatiwa kuwa ujenzi huo umechukua muda mrefu.

164. MHESHIMIWA DKT. REGINA CHRISTOPHER MALIMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali imejipangaje kuboresha Programu za Uanagenzi, Ufundi Stadi na Ubunifu ili kuwawezesha Vijana kujajiri na kuondoa changamoto ya ajira.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

165. MHESHIMIWA JESCA JOHN MAGUFULI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Vijana wanapata ujuzi sahihi na kunufaika kupitia Akili Mnemba (AI).

166. MHESHIMIWA THOMAS MGONTO KITIMA (IKUNGI MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itahakikisha kila Kijiji nchini kinapata mawasiliano ya kimtandao pamoja na Minara ili kurahisisha Mawasiliano.

WIZARA YA KILIMO:

167. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Kilimo:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Vihenge vya kisasa vya kutunzia nafaka vilivyopo eneo la TAZARA - Isangi Mbozi.

WIZARA YA MAJI:

168. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya Shilingi Bilioni 4.5 kwa Wananchi wa Mji wa Karatu ili waweze kupata huduma ya uhakika ya maji safi.

WIZARA YA FEDHA:

169. MHESHIMIWA LUTENGANO GEORGE MWALWIBA (BUSOKELO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka vivutio maalum vya kikodi kwa Vijana wanaoanza biashara ili kuchochea ajira na kukuza uchumi.

WIZARA YA UJENZI:

170. MHESHIMIWA YANNICK IKAYO NDOINYO (NGORONGORO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara kutoka Kigongoni hadi Wasso - Ngorongoro kwa kiwango cha lami.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

DODOMA
22 APRILI, 2026

BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE

